# ACHIEVERS FOCUS EXAMINATION SERIES

WEGO PUBLISHERS
*The achievers focus*

**STANDARD 8 – 2020**

**KISWAHILI**

AF0048N

**Muda: Saa 1 Dakika 40**

---

**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha kuchagua jibu lako lionyeshe katika **karatasi ya majibu** na wala **sio** katika kijitabu hiki cha maswali.
3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba karatasi ya majibu uliyopewa imejumuisha yafuatayo:

    **Namba Yako Ya Mtihani**
    **Jina Lako**
    **Jina La Shule Yako**

5. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
6. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usikunje.
7. Kwa kila swali 1 – 50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu **moja** tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
8. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano**

    **Katika Kijitabu cha Maswali:**

    21. Chagua jibu lenye ala za muziki pekee.
        A. filimbi, udi, mvukuto, chapuo
        B. njuga, tari, kinubi, fidia
        C. harimuni, marimba, msondo, maleba
        D. siwa, zeze, upatu, nembo

    Jibu sahihi ni **B**

    **Katika Karatasi ya Majibu:**

    1. [A] [B] [C] [D] 11. [A] [B] [C] [D] 21. [A] ~~[B]~~ [C] [D] 31. [A] [B] [C] [D] 41. [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 21, kisanduku chenye herufi B ndicho kilichochorwa kistari.

9. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako **kiwe cheusi** na kisijitokeze nje ya kisanduku.
10. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Website: www.achieversfocus.co.ke**
**Email: wegopublish@gmail.com**

**Jaza pengo kwa jibu lifaalo.**

Kenya ni mfano mzuri __1__ taifa lenye lugha nyingi zinazozidi __2__ za vikundi vidogo vidogo vya kikabila.Hapo kabla ya miaka mia moja hivi __3__ kila kimojawapo cha vikundi hivi __4__ kama taifa huru.Baada ya kuja kwa serikali ya kikoloni na __5__ baada ya Kenya kujinyakulia uhuru, haja __6__ kuunganisha raia wote chini ya taifa moja __7__ uongozi na __8__ moja lilikuwa ndilo jambo lililozingatiwa sana. __9__ utamaduni wa taifa la Kenya ni mchanganyiko wa tamaduni za watu wengi wenye mila, desturi, imani na itikadi __10__.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **1.** A. ya | B. wa | C. kwa | D. na |
| **2.** A. arobaini | B. arbaini | C. arubaini | D. arubaine |
| **3.** A. zilizopita | B. kulikopita | C. tuliyopita | D. iliyopita |
| **4.** A. kilijieleza | B. kilijitambulisha | C. kilijitanguliza | D. kilijisema |
| **5.** A. sanasana | B. kweli kweli | C. hasa | D. hasaa |
| **6.** A. za | B. ya | C. la | D. wa |
| **7.** A. kwenye | B. yenye | C. lenye | D. penye |
| **8.** A. shabaha | B. shabahaa | C. shabaaa | D. shabaa |
| **9.** A. Kwa hivyo | B. Kwa hio | C. Kwa hiyo | D. Kwa iyo |
| **10.** A. tafauti | B. utafauti | C. tofauti | D. utofauti |

__11__ hutumika __12__ kama njia mbadala ya kujihakikishia usalama.Hata hivyo kutokana na kuimarika kwa teknolojia na ujuzi wa hali ya juu itategemea aina unayotumia hususan __13__. Hivyo basi tunaweza kusema kuwa ni mfano wa mlinzi na pengine ndiyo sababu ya kitendawili __14__ __15__ mlangoni.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **11.** A. Vifuli | B. Makufuli | C. Kafuli | D. Vifuri |
| **12.** A. angalabu | B. aghalabu | C. angaa | D. agaa |
| **13.** A. vifunguo | B. kifunguo | C. funguo | D. vifungu |
| **14.** A. isemwavyo | B. kisemwavyo | C. kisemao | D. kisemwacho |
| **15.** A. askari | B. asikari | C. polis | D. asiikari |

**Kuanzia swali la 16 – 30 jibu kulingana na maagizo.**

16. Wachezaji wale ni kunguru hii ina maana kuwa
   A. hodari
   B. waoga
   C. wazembe
   D. wazuri

17. Ki hutumika kuonyesha yafuatayo isipokuwa?
   A. Masharti
   B. Ngeli
   C. Udogo
   D. Ukubwa

18. Neno kadamnasi lina silabi ngapi?
   A. 5
   B. 9
   C. 10
   D. 6

19. Bainisha kielezi katika sentensi ifuatayo.
   Aliingia darasani akampata mwanafunzi ameketi juu ya meza.
   A. juu
   B. meza
   C. darasani
   D. ya

20. Sayari ndogo sana kuliko zote ni
   A. Utaridi
   B. Sumbula
   C. Dunia
   D. Zebaki

21. Kanusha sentensi ifuatayo.
   Kulima ni kujitolea.
   A. Kutolima ni kujitolea
   B. Kulima si kutojitolea
   C. Kulima si kujitolea
   D. Kutolima si kutojitolea

22. Shaibu ni kwa ajuza ilhali _____ ni kwa koo
   A. mtamba
   B. mtetea
   C. jimbi
   D. shingo

23. Chagua wingi wa sentensi ifuatayo.
   Ukitaka kufuli na ufunguo tazama kabatini.
   A. Mkitaka vifuli na vifunguo tazameni makabatini
   B. Wakitaka makafuli na funguo tazameni kabatini
   C. Mkitaka makufuli na funguo tazameni makabati
   D. Mkitaka makufuli na funguo tazameni kabatini

24. Maneno yaliyopigwa mstari ni aina gani?
   <u>Lako</u> litatumika kubebea mzigo <u>wake</u>.
   A. Kielezi kivumishi
   B. Kivumishi kielezi
   C. Kiwakilishi Kivumishi
   D. Kivumishi Kiwakilishi

25. Andika sentensi ifuatayo katika hali ya wastani.
   Dudu liumalo silipe dole.
   A. Mdudu aumaye simpe kidole
   B. Kidudu kiumacho sikipe dole
   C. Mdudu aumaye simpe dole
   D. Vidudu viumavyo sivipe vidole.

26. Maneno yafuatayo yanafuatana vipi katika kamusi?
   (i) Muhibu
   (ii) Muhtasari
   (iii) Muhali
   (iv) Muhula
   A. (iii), (ii), (i), (iv)
   B. (iii), (i), (ii), (iv)
   C. (iv), (i), (ii), (iii)
   D. (iv), (ii), (i), (iii)

27. Chagua jibu lenye nomino zilizo katika ngeli ya I–I pekee.
   A. Kahawa, fedha
   B. Chumvi, chupa
   C. Mali, chai
   D. Sukari, mvua

28. Ni jibu lipi lenye maelezo sahihi?
   A. Muundi ni sehemu ya mkono kuanzia begani hadi kwenye kiwiko
   B. Kitengele ni sehemu ya mwisho ya mkono yenye vidole
   C. Nyonga ni sehemu ya juu ya kiuno
   D. Paji ni sehemu ya juu ya kichwa

**29.** Tikiti, limau na fenesi ni matunda ilhali ngano, shayiri na mchele ni
A. miti
B. vyakula
C. nafaka
D. mbegu

**30.** Chagua neno ambalo limetumia silabi changamano.
A. Mbuga
B. Kituta
C. Ziwa
D. Utulivu

**Soma taarifa kisha jibu maswali 31 – 40.**

Je, umewahi kutafakari kuhusu namna wanafunzi wengi, ukiwemo miongoni mwao, wanavyosafiri kwenda shuleni? Yamkini jibu lako kwa swali hili litadhihirisha kwamba asilimia kubwa ya wanafunzi hutembea kwenda shuleni, wengine hutumia baiskeli, magari ya umma na ya kibinafsi, pikipiki na garimoshi. Bila shaka aina ya usafiri hutofautiana kulingana na uwezo wa kiuchumi na umbali baina ya nyumbani kwa mwanafunzi na shule yake.

Kila aina ya usafiri ina changamoto maalum. Mathalani ikiwa umezungumza na wenzako ambao hutembea kwenda shuleni, haikosi wamekuelezea dhuluma wanazokumbana nazo. Licha ya safari za aina hii kuwachosha wanafunzi, ni wazi kuwa Wanafunzi wengine hata hukosa masomo kwa sababu ya kutopitika kwa njia wakati wa mvua nyingi. Pengine hata wewe umewahi kujipata katika njia panda baada ya daraja unalovukia kusombwa na maji ya mto uliofurika. Isitoshe, watembeao huweza kuathirika kiafya wakati wa kipupwe. Baridi huweza kuwasababishia pumu au hata kichomi. Wengine huwa katika hatari ya kuteleza kwenye njia zenye matope na kuvunjika viungo vya mwili. Hawa pia wamo katika hatari zaidi ya kutekwa nyara na hata kunyanyaswa kimapenzi.

Wanafunzi wengine **huwahusudu** wale ambao husafiri shuleni, ama kwa gari la shule, au la kibinafsi. Wakiulizwa kuhusu kiini cha husuda hii, wanasema kwamba Wenzao hawa hawachoki kwani magari haya yanawachukua kutoka malangoni mwa nyumba zao. Hata hivyo, ukichunguza vyema utapata kwamba hata hawa wana matatizo sugu. Kwa vile magari ya shule huwabeba wanafunzi kutoka sehemu mbalimbali, magari haya hayana budi kuanza safari mapema. Hili huwalazimu wanafunzi nao kuamka alfajiri na mapema ili kuyawahi magari haya. Matokeo ni kwamba Wanafunzi wengi hawadiriki kulala usingizi wa kutosha. Kuna wale ambao hulala saa nne usiku baada ya kukamilisha kazi za darasani, kisha wanaraushwa saa kumi ili kujitayarishia basi la saa kumi na moja. Wanafunzi wa aina hii hukumbwa na uchovu, na bila shaka husinzia darasani.

Isitoshe, wanafunzi wanaotumia usafiri wa umma hulalamikia msongamano wa magari ambao unawafanya kukawia njiani, na hata kupewa adhabu kwa kuchelewa kufika shuleni. Wengine hata hukataliwa na magari ya abiria, eti wanalipa fedha kidogo, na kuwasababishia Wenye magari hasara. Wanafunzi hawa huaibika na kulazimika kutembea hadi shuleni. Hali kadhalika, magari ya umma humpa mwanafunzi mazingira ya kujifunzia tabia; nzuri na mbaya. Pamoja na Wanafunzi hawa kupata fursa ya kutangamana na wenzao kutoka shule nyingine, wao pia huweza kuathiriwa vibaya na hulka za wasafiri wengine. Kuna Wale ambao huiga lugha, mitindo ya mavazi, namna ya kutembea, na hata mienendo mingine ya madereva na utingo. Wengine huishia kuwa waraibu sugu Wa vileo kutokana na vielelezo wanavyopata kwenye magari haya. Muziki, picha za video, na mazungumzo kupitia vyombo vya habari vilivyo kwenye magari haya huchangia kuzorotesha tabia ya wanafunzi. Hii ni kwa sababu baadhi ya masuala yanayozungumziwa ni ya aibu na hayapaswi kusikilizwa na watu wa umri mbichi.

Ni dhahiri kwamba kila aina ya usafiri ina athari zake, Hata hivyo, baniani mbaya kiatu chake dawa. Usafiri unahitajika katika kufanikisha masomo ya wanafunzi, na katika uchukuzi wa bidhaa na vifaa mbalimbali ambavyo wanahitaji shuleni. Ni jukumu la kila mwanajamii kuhakikisha kwamba mikakati ifaayo imewekwa ili kukinga dhidi ya madhara yanayoandamana na kila aina ya usafiri. Wanafunzi nao wakae ange kutambua watu ambao huenda wakawatosa katika maovu. Wachuje ya kuiga na ya kukataa.

**31.** Kulingana na aya ya kwanza
A. wanafunzi wengi huabiri vyombo vya usafiri ili kufika shuleni
B. anayeenda kwa kawaida huwazia njia yake ya usafiri.
C. uchaguzi wa njia ya usafiri hutegemea masafa kati ya anakoishi mwanafunzi na anakosomea
D. wale walio na pesa kidogo hulazimika kutumia magari ya umma na baiskeli

**32.** Chagua jibu lisilo sahihi kulingana na kifungu.
A. Matatizo ya usafiri hutofautiana kulingana na aina ya usafiri
B. Barabara mbaya huweza kualhiri utendaji wa wanafunzi klelimu
C. Mwandishi ana hakika kwamba msomaji ameambiwa yanayowapata wenzake
D. Magonjwa mengine huweza kutokana na hali ya anga

**33.** Chagua madhara ya aina ya usafiri unaozungumziwa katika aya ya pili.
A. Mvua nyingi, kutatizika kimawazo
B. Kupatwa na ajali, kuchukuliwa kwa nguvu
C. Kuharibika kwa daraja, majira ya baridi
D. Ulemavu mwilini, kuingiliana na mazingira yasiyovutia

**34.** Aya ya tatu imebainisha kwamba wanafunzi wengine
A. wangetaka aina ya usafiri unaohusu nyumbani kwao
B. wanadhani kwamba wanaosafiri kwa magari hawasumbuki
C. wanapenda hali ya usafiri usiomhitaji mtu kutumia nguvu
D. wanaona kwamba wanaomiliki magari huwa na matatizo mepesi

**35.** Ni jibu lipi sahihi kulingana na aya ya tatu?
A. Kutumia gari moja kusafira humnyima mwanafunzi mapumziko yafaayo
B. Magari yakianza safari shuleni mapema huwafanya wanafunzi kumaliza kazi mapema
C. Wanafunzi wakichoka hushindwa kuona umuhimu wa masomo darasani
D. Kupitia sehemu mbalimbali za gari humfanya mwanafunzi kuraushwa

**36.** Kulingana na aya ya nne
A. usafiri wa umma huwafanya wanafunzi kulaumiana
B. wanafunzi wengi hawafurahishwi na hali ya magari kuchelewa nyumbani
C. msongamano wa magari huweza kuathiri utulivu wa wanafunzi shuleni
D. wanafunzi hupuuzwa garini na waliokosa nauli

**37.** Maana ya methali, "Hakuna masika yasiyokuwa na mbu" imejitokeza katika kifungu kwani magari ya umma
A. huwaletea wenye magari hasara, huonyesha mienendo mizuri
B. hushusha hadhi ya wanafunzi, huonyesha namna ya kuwasiliana
C. hukuza ushirikiano wa kijamii, hupalilia kuzorota kwa maadili
D. huwaongezea wanafunzi maarifa, huharibu namna ya kujipamba

**38.** Aya ya nne imebainisha kwamba
A. wale wanaokuwa waraibu zaidi ni wale ambao wanaingiliana sana na madereva
B. jinsi mtu anavyotembea hulingana na tabia zinazosababishwa na mienendo ya utingo
C. mazungumzo kwenye magari ya abiria yanataka kumjengea mwanafunzi hali yenye vielelezo vyema kwao shuleni
D. hulka ya mwanafunzi huweza kuathirika vibaya anapopata maarifa yasiyolingana na mahitaji ya rika lake

39. Mtazamo wa mwandishi katika aya ya mwisho ni kwamba
  A. Wanafunzi wakiwa makini wanaweza kujiepusha na madhara ya usafiri
  B. Wasafiri wakijua hasara za safari wataimarisha juhudi za kusoma
  C. Wanajamii wakitumia njia zifaazo shule zitapata vifaa vinavyohitajika
  D. Watu wakizifahamu tofauti za usafiri watapimguza maovu kwa wasomao

40. Maana ya '**huwahusudu**' kulingana na kifungu ni
  A. huwapenda kwa hali yao
  B. huvutiwa na hali yao
  C. huwafikiria kwa hali yao
  D. huhimizwa na hali yao

**Soma kifungu hiki kwa makini kisha ujibu maswali 41 – 50.**

Msemo, "Vijana ndio viongozi wa kesho", hutolewa na wengi bila kuwazia maana yake. Hata hivyo, ni dhahiri kwamba mtu **anapoupigia darubini** msemo huu, utamwelekeza kugundua kuwa vijana ni mbegu ambayo inahitaji kupaliliwa ili kukifaa kizazi chao na cha siku za usoni. Tunaposema kwamba vijana ni viongozi wa kesho, tunamaanisha kwamba vijana ndio wanaotarajiwa kuchukua usukani wa kuidhibiti jamii yao wakati utendakazi wa watangulizi wao unapofikia kikomo kutokana na umri au maradhi.

Ni muhimu kujiuliza, "Ni kwa vipi vijana wanaweza kuwa tegemeo la kesho?" Kwanza kabisa, ibainike kwamba vijana, kwa sababu ya umri wao mbichi, wana mifupa myepesi, hivyo utendakazi wao huwa bora kuliko wa watu wa makamo au wale waliobugia chumvi nyingi. Isitoshe, kwa sababu ya bongo zao kuwa changa, vijana huweza kujifunza kwa urahisi mbinu mpya na bora za kuendeleza nchi.

Bila shaka ukitazama katika mazingira yako, unapata kwamba aghalabu vijana ndio wenye ustadi wa hali ya juu katika kutumia teknolojia ya kisasa. Hali hiyo inachangia kuimarisha ubunifu na kuboresha hali ya maisha.

Sijui kama unafahamu kwamba ile huduma ya simu almaarufu MPESA ambayo imeifanya Kenya kutia fora kitaifa na kimataifa ilibuniwa na kijana. Hali kadhalika, vijana wana nafasi kubwa katika kuendeleza maaadili na mshikamano wa kijamii. Kundi hili lina ushawishi mkubwa kwa raia.

Kwa vile vijana ndio wengi nchini, wanaweza kuifikia asilimia kubwa ya raia na kuiathiri, ama kwa njia hasi, au chanya. Si ajabu kupata kwamba mizozo mingine nchini, japo huenda inazuliwa na wazee, hupaliliwa na kuendelezwa zaidi na vijana waliopotoshwa na wazee hawa.

Isitoshe, kwa vile vijana wanaaminiana na kuthaminiana sana, wao wanaweza kusaidia kubadili mienendo ya wenzao. Ukichunguza katika jamii unamoishi, utapata kwamba vijana wengi huhiari kuwafichulia wenzao siri zao badala ya wazazi wao. Hili labda husababishwa na tofauti za kiumri na kimtazamo kati ya vijana na wazazi, au kile vijana wanachokiita, '**ukali wa wazazi**'.

Kwa sababu ya kuaminiana kwa vijana, utapata kwamba vijana wengi wameweza kuwashauri wenzao dhidi ya kuchukua hatua zisizo za busara kama vile kujiingiza katika ndoa za mapema, kushiriki mapenzi kiholela na hata kujitia kitanzi.

Umuhimu wa vijana hauwezi kupuuzwa. Licha ya kwamba wao ndio wanotarajiwa kuklendeleza kizazi cha jamii yao, wao ndio wanorithishwa desturi za jamii yenyewe ili kuziendeleza. Ni jukumu la wanajamii kuhakikisha kwamba wamewatayarisha vijana kukabiliana na majukumu yao.

Jamii haina budi kuhakikisha kwamba asilimia kubwa ya vijana imepata elimu ili kupata stadi za kuzalisha mali na kuendeleza uongozi ufaao.

Kadhalika, ni muhimu kuhakikisha kwamba vijana hawabakii tu kuwa viongozi wa kesho katika kauli na maandishi yetu. Washirikishwe katika uongozi wenyewe wakiwa wadogo ili ifikapo wakati wa kuzichukua nyadhifa za ngazi za juu waweze kuzimudu ipasavyo. Wanaotumia msemo, viongozi wa kesho kumaanisha kwamba vijana hawana nafasi katika uongozi wa sasa nao waonywe dhidi ya haya.

Wakumbushwe kuwa iwapo watang'ang'ania kubaki uongozini hata wanapofikia umri wa kustaafu, wanaendelea kuua ari ya vijana ya kuwajibikia uongozi wa jamii yao.

**41.** Kulingana na kifungu, vijana ndio viongozi wa kesho kwani wao
- A. wakiheshimiwa vizuri wataweza kuanzisha kizazi kijacho
- B. wakitayarishwa vyema wanaweza kuiletea jamii neema baadaye
- C. wakitambuliwa ipasavyo wanaweza kuifahamisha jamii faida yao baadaye
- D. wakiamuliwa ipasavyo, wanaweza kuandaliwa mamlaka yajayo

**42.** Aya ya kwanza imeonyesha kwamba
- A. umri na hali ya afya ya mtu huathiri matokeo ya kazi yake
- B. kutokuwepo kwa vijana hupunguza matumaini ya kurithi mamlaka
- C. kutowafikiria vijana hudhoofisha uongozi unaotangulia
- D. unyonge wa mwili huathiri kubadilishana kwa zamu kazini

**43.** Katika jamii yenye watu wachanga
- A. njia mpya za kukabiliana na umri hustawishwa
- B. udumishaji wa teknolojia ya kisasa huwa maarufu
- C. mikakati bora ya kufanikisha maendeleo huanzishwa
- D. hali ya kubuni mitandao huwa ya kimataifa

**44.** Kulingana na aya ya tatu
- A. mizozo ya wazee waliopotoka hutangazwa zaidi na vijana
- B. vijana hufichua siri za wengine kuliko wazazi wao
- C. kuaminiana miongoni mwa vijana huwafanya wengine wasiuawe
- D. vijana ndio wanaoweza zaidi kuendeleza matendo mema katika jamii

**45.** Vijana wanaweza kuleta mapinduzi yafaayo nchini kwa vile
- A. mizozo inapoanzishwa wao huwa na ushauri tofauti
- B. siri zinapotokea nyumbani wao huwafichulia wenzao
- C. wanapendana na kujitambulisha na kila mmoja wao
- D. wanafunzana na kuelewa tofauti za wazazi

**46.** Chagua jibu lisilo sahihi kwa mujibu wa kufungu. Vijana
- A. wanawaogopa wazazi wao kwa vile watu wanajua ni wakali
- B. huwaficha wazazi mambo kwa sababu ni wa kizazi kingine
- C. wanachangia katika utoaji nasaha katika jamii
- D. wanaweza kubadilisha na kuyaokoa maisha ya wenzao

**47.** Mwandishi ameonyesha kwamba vijana ndio
- A. wanaopaswa kuanzisha elimu ya jamii
- B. wanaopitisha matendo na imani za jamii
- C. wanaotarajiwa kuhusiana na vizazi
- D. wanaowaonyesha mbinu za kutafuta mali kwao

**48.** Chagua maana ya '**anapoupigia darubini**'.
- A. anapousisitiza kwa uaminifu
- B. anapouelewa kwa dhati
- C. anapoufafanua kwa mapana
- D. anapouchunguza kwa kina

**49.** Kulingana na aya ya mwisho kufanikiwa kwa vijana kunategemea

A. kupewa majukumu ya uongozi wakiwa wachanga
B. muda wanaochukua kufunzwa uongozi na jamii
C. kustaafu uongozini kwa wazee wenye busara
D. hamu wanayopata baada ya kuchukua uongozi

**50.** Wanachokiita '**ukali wa wazazi**' ina maana kwamba mwandishi

A. anakana kuwa wazazi ni wakali
B. anahofia kuwa wazazi ni wakali
C. anadai kuwa wazazi ni wakali
D. ameamini kuwa wazazi ni wakali